

(*Masomo maalumu kwaajili ya watumishi*).

Kama Mhubiri au Mtumishi wa Mungu, usiupende ulimwengu wala usiikimbia sauti ya Mungu.

Bwana YESU alimwambia Petro maneno haya...

Luka 5:10 “na kadhalika Yakobo na Yohana, wana wa Zebedayo, waliokuwa washirika wa Simoni. Yesu akamwambia Simoni, Usiogope, TANGU SASA UTAKUWA UKIVUA WATU”.

Hapa tunaona Bwana YESU anawafananisha “**watu**” na “**samaki**”...na “**dunia**” anaifananisha na “**bahari**”...

Tena anazidi kulithibitisha hili katika *Mathayo 13:47- 49..*

*Mathayo 13:47 "Tena ufalme wa mbinguni umefanana na juya,
lililotupwa baharini, likakusanya samaki wa kila namna;*

*48 hata lilipojaa, walilivuta pwan; wakaketi, wakakusanya walio
wema vyomboni, bali walio wabaya wakawatupa*

*49 Ndivyo itakavyokuwa katika mwisho wa dunia; malaika
watatokea, watawatenga waovu mbali na wenye haki,"*

Kama samaki wanawakilisha watu waliopo duniani, basi Injili ya **BWANA YESU ndio NYAVU** na Bwana amekusudia tuwavue watu (*samaki*) kutoka katika dunia, na si samaki watuvue sisi na kutushusha baharini. Maana yake samaki wanatakiwa wbolewe kwenye maji, na si samaki watuvute sisi majini.

Utauliza je! MHUBIRI anaweza kuvuliwa na samaki?.. jibu ni NDIO!

Utakumbuka kisa cha YONA? Alipoikimbia sauti ya BWANA, ni nini kilitokea?, biblia inasema ALIMEZWA na samaki na akakaa tumboni mwa samaki siku tatu.

Yona 1:17 "Bwana akaweka tayari samaki mkubwa ili ammeze Yona, naye Yona akawa ndani ya tumbo la samaki yule muda wa siku tatu, mchana na usiku"

Vile vile, na mtumishi/mhubiri anayeikimbia sauti ya Mungu, kitakachofuata ni **KUMEZWA NA WATU WA ULIMWENGU**, (*Mtu huyu anawekwa mikononi mwa watu wakuu wa ulimwengu*) ambao hawana huruma, wenye nguvu kuliko yeye.

Tumbo la samaki ni vifungo vyote vyatya mateso vyatya watu wa kidunia,

Je wewe ni Mhubiri??...Isikie sauti ya Mungu, simama hubiri Neno la Mungu, usiende njia ya bahari (ya ulimwengu)...Ukienda njia ya ulimwengu *ya bahari* iwe kwa lengo la kuhubiri sio kwa kufuata mambo yako, kwani bahari ina hatari nyingi.

Usiwe kama Nabii Yona ambaye aliikimbia sauti ya Mungu na kwenda njia ya bahari, na akapata ajali ile.

Bwana atusaidie sana.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kupofya link hii >>

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Kwa mawasiliano: +255789001312 au +255693036618

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

UNAMCHUKULIA YESU KWAKO KAMA NANI?

[Makasia ni nini? \(Yona 1:13\).](#)

[MADHARA YA KUTAFUTA ISHARA.](#)

VUA SAMAKI, NA SAMAKI WASIKUVUE WEWE.

TWEKA MPAKA VILINDINI.

NI MAJIRA YAPI YA NEEMA WEWE UPO?

Rudi Nyumbani

Share on:

WhatsApp

[Print this post](#)